

## **WAZIRI SIMBAWENE; MFUMO WA KIELEKTONIKI WA USIMAMIZI WA KESI NI USHINDI KATIKA KUTENDA HAKI KWA WANANCHI**

**Na. Lusungu Helela-Dodoma**

**24 Agosti 2023**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. George Simbachawene amesema kitendo cha Serikali kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa kesi (CMIS) uliouunganisha taasisi zote za haki jinai ni ushindi mkubwa sana katika kutenda haki kwa Wananchi

Mhe. George Simbachawene ameyasema hayo leo Jijini Dodoma kwenye uzinduzi wa mfumo huo ultiotengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Amesema mfumo huo umekamilika katika wakati sahihi ambapo Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anaendelea na jitihada za kuimarisha utoaji haki kwa wananchi.

Amesema Mfumo huu umeunganishwa na mfumo mkuu wa serikali wa kubadilishana taarifa na mifumo ya baadhi ya Taasisi za Haki Jinai kama vile Polisi, Takukuru na Mahakama, ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais Mhe. Samia kuhusu mifumo ya serikali kubadilishana taarifa.

Amesema hadi sasa kesi za jinai 17,411 zimesajiliwa kwenye mfumo huo na kati ya hizo 7,361 zimeshafika mwisho na kutolewa hukumu na 10,050 zipo hatua mbalimbali za maamuzi.

Mhe. Simbachawene ametumia fursa hiyo kuzihimiza Taasisi nyingine za Umma ambazo bado zina kiwango kidogo cha utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao kuongeza matumizi ya Tehama ili kuongeza ufanisi na kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.

Naye, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Pauline Gekul, amesema wizara ya Katiba na Sheria imejizatiti kuimarisha jitihada za kuhakikisha inatengeneza mifumo madhubuti ya Tehama ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Utumishi, Bw, Xavier Daudi amesema kuzinduliwa kwa mfumo huo ni hatua kubwa katika kuhakikisha haki inatendeka kwa wananchi kwani jambo hilo halikuwa rahisi kufanyika kwa siku za nyuma

” Mfumo huu unafungua ukurasa mpya katika kuelekea uchumi wa kidigitari huku tukifanikisha azma ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha mifumo yote ya utoaji haki inasomana ” amesema Naibu Katibu Mkuu, Bw. Daudi

Awali, Mkurugenzi wa Mashtaka, Sylvester Mwakitalu, amesema mfumo huo utatunza kumbukumbu zote ikiwamo hati za mashtaka na hukumu na utakuwa na uwezo wa kuonesha jalada lipo kwa Wakili gani na limechukua muda gani.

Kadhalika, Mkurugenzi Mkuu wa eGA, Benedict Ndomba, amesema kuzinduliwa kwa mfumo huo ni utekelezaji wa dhamira ya serikali ya kuboresha mifumo ya utendaji kazi.

Mwisho.